# Sisi ni wa muhimu

# Tuthamini

## Orodha ya ukaguzi kwa vijana Wanaofanya kazi na mashirika



MTANDAO WA KIMATAIFA
WA VIJANA WANAOISHI
NA VVU

# KUPIMA JINSI MASHIRIKA YALIVYO VIZURI KUSHIRIKISHA VIJANA WANAOISHI NA VVU

1 = Mbaya  2 = Chini ya Wastani  3 = Wastani  4 = Nzuri  5 = Bora sana







## KUWAWEKA VIJANA SALAMA

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Shirika lina sera ya ulinzi. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 2 | Wafanyakazi wamepewa mafunzo juu ya umuhimu wa sera ya ulinzi kwa vijana na wajibu wa kuitunza. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 3 | Shirika lilifanya tathmini ya hatari kwa shughuli za moja kwa moja na vijana kutambua hatari kubwa na hatua za kupunguza hatari na madhara. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 4 | Umefahamishwa kuhusu hatua shirika linachukua kuzuia au kupunguza hatari na madhara kwa vijana wanaofanya kazi nao. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 5 | Ulipewa habari na mafunzo juu ya sera ya ulinzi na usalama kwa taratibu za kusafiri na kuripoti. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 6 | Shirika limejadili jinsi watakavyotumia habari na data yako na wameuliza kibali chako. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 7 | Shirika limekupa msaada wa vitendo wa kibinafsi ili kulinda afya yako na ustawi kupitia ushauri, mawasiliano au kusaidiana nao. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |

## KUTHAMINI MCHANGO WA VIJANA

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 8 | Shirika liliwasiliana nawe, unaelewa wao ni nani, wanafanya nini na jinsi gani unaweza kufanya nao kazi. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 9 | Shirika lilitenga bajeti kukusaidia, ama kupitia ruzuku au msaada kwa shirika unaloshirikiana nalo, kwa kutoa vitu kama pesa ya kujikimu, posho ya siku au udhamini. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 10 | Shirika lilionyesha wazi kujitolea kufanya kazi na wewe, na uwazi kuhusu kazi utakayofanya na matarajio. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 11 | Shirika lilikushirikisha wewe na vijana wengine katika kila hatua ya mradi. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 12 | Shirika limetoa nafasi kwa vijana kuongoza kazi na kufanya maamuzi ambayo yana athari (matokeo) na kuleta mabadiliko. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 13 | Shirika lilithamini juhudi zako na lilikufanya uhisi kuhusika, kuheshimiwa na kuthaminiwa. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |

## KUHAKIKISHA UWAKILISHI WA MAKUNDI MBALIMBALI YA VIJANA

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 14 | Shirika limehakikisha linafanya kazi na vijana wa makundi mbali mbali, kuongeza uwakilishi mpana kwa kuondoa vikwazo vya ushiriki wa vijana – kama vile ufikiwaji, eneo, uhalifu, lugha. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 15 | Shirika limetenga muda na fedha kuwafikia vijana kutoka jamii mbalimbali zaidi kwa uwakilishi wa kweli. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 16 | Shirika limehakikisha maombi kwa vijana kuchukua nafasi katika kushiriki kwenye shughuli za sera, utetezi au programu yanatangazwa kwa uwazi. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 17 | Shirika limechunguza njia za ubunifu za kuwashirikisha vijana wengine ambao kwa kawaida halifanyi nao kazi, kwa kutumia majukwaa ya mtandaoni, zana za kidijitali. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 18 | Shirika limejenga ushirikiano na mashirika yanayoongozwa na vijana ili kusaidia zaidi uwakilishi wa vijana. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |

## KUTOA MSAADA

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 19 | Shirika lilijadiliana nawe kuhusu tukio au kipande cha kazi mapema ikijumuisha malipo, kusafiri na vifaa kabla ya kukuuliza kukubali. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 20 | Shirika lilisaidia gharama zote za usafiri - visa, kwenda ubalozi, bima, chanjo, kuunganisha safari za ndege, posho ya siku na malipo yote hutayarishwa mapema. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 21 | Shirika lilikulipa kupitia pesa ya kujikimu, posho, data na vocha za simu, ufadhili wa mashirika. Walijadiliana nawe ili kuchunguza unachohitaji. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 22 | Mashirika yalitoa pesa mapema, kwa hiyo una pesa za kusafiri nazo na huna inatarajiwa kulipa mbeleni. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 23 | Shirika lilitoa taarifa juu ya nchi mpya, juu ya usalama, utamaduni, lugha, fedha. Wamehakikisha una bima na maelezo kuhusu usalama. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 24 | Shirika lilitoa usaidizi katika mikutano na matukio na tafsiri muhimu inapohitajika ili kukuruhusu kushiriki katika sehemu zote za tukio. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 25 | Shirika lilitambua ustawi wa vijana na hawakuwapa vijana kazi nyingi zaidi ya uwezo wao ili kuondoa hatari ya kuchoka. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |


## KUJENGA USHIRIKIANO MZURI BAINA YA VIJANA

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 26 | Shirika lilitoa mafunzo kwa wafanyakazi jinsi gani kufanya kazi kwa ufanisi na vijana ikiwemo kuchunguza mitazamo na maadili, changamoto na mienendo ili kuunda ubia sawa zaidi. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 27 | Shirika lilitoa nafasi na taratibu ili utoe maoni na changamoto za shirika bila hofu ya kukataliwa au kutengwa. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 28 | Shirika lilitoa nafasi salama kwa ajili yako kusema maneno yako mwenyewe na kuleta mawazo yako mwenyewe, hawakushurutisha uzungumze mambo ambayo huna raha nayo. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 29 | Shurika liliunga mkono mashirika yanayoongozwa na vijana na kuamini uwezo wao wa kufanya kazi kwa usimamizi sahihi. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 30 | Shirika liliwezesha kukuunganisha na mashirika na mitandao tofauti bila kuunda ushindani au kuweka mipaka ya mahusiano yako na mashirika mengine. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |

| KUWEKEZA KATIKA UENDELEVU WA MASHIRIKA YANAYOONGOZWA NA VIJANA | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 31 | Shirika lilipanga kufanya kazi kwa muda mrefu na vijana na sio matukio ya mara moja tu. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 32 | Shirika lilitengeneza njia kwa vijana ndani ya shirika na kutambulisha majukumu na hatua za maendeleo. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 33 | Shirika liliwekeza katika kujenga ujuzi na ushauri kwako na kwa vijana wengine na kukutayarisha kwa kazi ya sasa na ya baadaye. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 34 | Shirika lilifanya mpango kwa ajili ya vijana wanaovuka kutoka sekta ya vijana na kuwekeza katika kizazi kijacho cha vijana. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 35 | Shirika lilihakikisha kuwa matarajio ya vijana yanakuwa halisi na hawakuhatarisha kukulemea. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 36 | Shirika liliandika na kukuzwa thamani ya kazi zao na vijana na liliripoti kwa wafadhili juu yake na kutetea uwekezaji mkubwa katika ushirikiano wa vijana na watu wazima. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |

| KUENDELEZA UWAJIBIKAJI MKUBWA KWA VIJANA | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 37 | Shirika lilikusanya ridhaa kutoka kwa vijana baada ya kufahamishwa juu ya kazi na matumizi ya picha zao na habari katika nyenzo yoyote, makala, au maudhui ya mtandao. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 38 | Shirika lilitengeneza taratibu za kupata maoni kutoka kwako na vijana wengine ushiriki wako na, kutathmini jinsi ulivyoungwa mkono na jinsi ulivyojisikia. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 39 | Shirika lilihakikisha kwamba linakupatia maoni juu ya matokeo na mchango uliotoa uliposhiriki katika kazi | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 40 | Shirika lilikupa marejeleo, pongezi, barua za msaada kwa kazi yako. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 41 | Shirika lilihakikisha pindi ulipofanya kazi nao, ulihusika kujifunza mafunzo endelevu na maendeleo yako kwa kazi za baadae. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 42 | Shirika lilikuuliza kutathmini kazi yao juu ya ushiriki wa maana na wa kimaadili ili ili kuendelea kuboresha. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |

# ULIFANYAJE?



**Chini ya 90**

Shirika hili halizingatii jinsi ya kufanya kazi na vijana kwa njia ya ‘maana na kimaadili’. Unapaswa kutafakari kwa makini juu ya ushiriki wako.



**90 - 130**

Shirika hili linachukua baadhi ya hatua za kuunga mkono vijana kwa njia ya ‘maana na kimaadili’. Unapaswa kukagua alama katika maeneo maalumu na kuzingatia kama unafurahi kufanya kazi na yao. Unaweza kupendekeza **mwongozo** kwa shirika ili kuwasaidia kuboresha.



**130 - 170**

Shirika hili linafanya vizuri kwa kujihusisha na vijana katika njia ya ‘maana na kimaadili’ lakini bado kuna zaidi wanaweza kufanya. Fikiria jinsi unavyoweza kuwasaidia kuboresha katika maeneo yenye alama za chini.



**170 - 210**

Shirika hili linafikiria kwa makini jinsi ya kufanya kazi na vijana katika njia ya 'maana na maadili' na wameonesha mambo yako salama ili kuhakikisha vijana wanaungwa mkono, wanathaminiwa na kuheshimiwa. Daima ipo nafasi ya kuboresha zaidi lakini hili ni shirika linaloongoza.

Global Network of Young People Living With HIV
Eerste Helmersstraat 17 B3
1054 CX Amsterdam, Netherlands
T: +31 (20) 423 4114
E: info@yplusglobal.org

Iliyochapishwa: Februari 2022
© 2022 The Global Network of Young People
Living with HIV (Y+ Global)
Kubuni Mpangilio: Garry Robson
Vielelezo © Garry Robson

Rasilimali za Sisi Ni Wa Muhimu, Tuthamini:
www.yplusglobal.org/resources/we-matter-value-us

www.yplusglobal.org



@YplusGlobal

@Yplus_global

uplus_global

Y Plus Global

# Sisi ni wa muhimu

# Tuthamini

MTANDAO WA KIMATAIFA
WA VIJANA WANAOISHI
NA VVU